**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# Misungwi Community Development Technical Training Institute
# (Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi)

S.L.P 2799 Mwanza| Baruapepe: pmissungwi@jamii.go.tz| Tovuti:www.misungwicdtti.ac.tz

**Kumb.Na: IMJ/CDTTI/T.10/601** **04 Agosti, 2024**

**Ndugu Mwanafunzi,**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA CHETI CHA AWALI KATIKA FANI YA UHANDISI UJENZI NA MAENDELEO YA JAMII (BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN CIVIL ENGINEERING WITH COMMUNITY DEVELOPMENT - NTA LEVEL 4) MWAKA WA MASOMO 2024/2025**

Ninayofuraha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na programu ya Uhandisi Ujenzi na Maendeleo ya Jamii NTA Level 4 inayotolewa chuoni (Misungwi CDTTI). Mafunzo haya ni ya miaka mitatu ambapo kila mwaka unajitegemea. Endapo utafaulu mwaka wa kwanza na kukubali kuendelea mwaka wa pili – NTA Level 5 (Technician Certificate) utasoma kwa mwaka mmoja pia na ukifaulu utaendelea na mwaka wa tatu NTA Level 6 (Ordinary Diploma) kwa muda wa mwaka mmoja ndipo utakua umekamilisha miaka mitatu.

Chuo kitafunguliwa tarehe **07 Oktoba, 2024** na unapaswa kuyasoma maelekezo kwa makini sana kabla hujafika chuoni

Baada ya kuwasili utapewa Sheria Ndogo za Wanafunzi, ambazo zinashughulikia kwa ukamilifu kanuni zinazosimamia kukaa kwako Misungwi CDTTI

## MAELEKEZO YA JUMLA

### 1. Mahali chuo kinapopatikana (Misungwi CDTTI).

Chuo kipo Wilaya ya Misungwi Kata ya Misungwi Kijiji cha Old Misungwi Kitongoji cha Mitindo na kilomita 45 kusini kutoka Mwanza jiji na takribani mita 800 mashariki kutoka barabara ya Mwanza-Shinyanga na karibu na Shule ya Msingi Mitindo.

Ili kufika Misungwi CDTTI kutoka Mwanza, utalazimika kupanda basi la abiria kutoka stendi ya mabasi ya Mwanza mahususi katika kituo cha Buhongwa/Nyashishi. Mabasi ya abiria hufanya kazi kila siku hadi 2:00 usiku na gharama ya sasa kwa kila abiria ni TZS.1, 500/= kwa safari. Kwa anaetokea barabara ya shinyanga-mwanza anaweza kushuka standi ya misungwi na kuchukua usafiri wa bodaboda hadi chuoni na utamgharimu TZS 1000/=.

### 2. Utaratibu wa Malipo

Wanafunzi wote wanatakiwa kulipa ada zao kupitia namba ya Malipo (Control Number) itakayotolewa chuoni. Maelezo mengine yanapatikana katika muundo wa ada uliyoambatanishwa kwenye fomu hii.

Hakuna mwanafunzi atakayesajiliwa isipokuwa awe ameleta risiti ya malipo (pay in slip) kama ushahidi wa malipo ya ada siku ya usajili na pesa taslimu mkononi ni marufuku kabisa.

### 3. Kuwasili Misungwi CDTTI

Unapaswa kufika Misungwi CDTTI kabla ya tarehe 21 Oktoba,2024 . Tafadhali fanya mipango yako ya usafiri ili kukuwezesha kusafiri hadi Misungwi CDTTI. Unapaswa kukidhi gharama zote za usafiri peke yako na hakutakuwa na marejesho.

### 4. Usajili

Utahitajika kujisajili Misungwi CDTTI. Usajili huu utafanyika katika wiki ya tarehe **07 Oktoba, 2024** kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi 10.30 jioni. Fomu ya Usajili wa Mwanafunzi itatolewa kwa ajili ya kuijaza na kuiwasilisha kwa Afisa udahili ana kwa ana. Usajili uliochelewa hautaruhusiwa.

Kwa madhumuni ya usajili, unatakiwa kuleta picha mbili za pasipoti za hivi karibuni, **Namba ya NIDA ya Mwanafunzi (Ni lazima kwa alietimiza miaka 18 kwa ajili ya Bima ya Afya)** na vyeti/nakala. Kutofanya hivyo kutasababisha kufutiwa Usajili Misungwi CDTTI.

Tafadhali pia kumbuka kuwa uwasilishaji wa vyeti vya kughushi utasababisha kufutwa kwa usajili na hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi ya mhalifu.

### 5. Wiki ya Maelekezo (Orientation Week)

Kuanzia tarehe 14 – 18 Oktoba, 2024 kutakua na maelekezo ya kufahamu Chuo, Programu na Mazingira yote ya chuo kwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Misungwi CDTTI. Wanafunzi wote wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika programu elekezi. Taarifa zaidi kuhusu programu hii utapewa ufikapo Misungwi CDTTI . Kutoshiriki katika mpango wa maelekezo kunaweza kusababisha kutosajiliwa.

### 6. Mahudhurio Darasani

Wanafunzi wa Misungwi CDTTI wanatakiwa kuhudhuria angalau asilimia 75 ya mihadhara, semina na Mafunzo kwa vitendo vyote ili kupata sifa za kufanya mitihani ya Mwisho wa Muhula. Mwanafunzi anaweza kupata likizo ya kutokuwepo kwa muda usiozidi siku 5 wakati wa muhula baada ya kutuma maombi kwa Mkuu wa Chuo. Maombi haya yataambatana na idhini iliyotiwa saini ya Msimamizi wa Darasa na Mwadili wa Wanafunzi.

### 7. Makazi, Malazi na Chakula ( Meals and Accommodation)

Taasisi ina ukomo wa malazi ndani ya chuo ambayo yametengwa kwa kuongozwa na Sera ya Malazi ya Chuo inayotoa kipaumbele cha wasichana na wavulana watakaowahi kufika chuoni na watu wenye mahitaji maalum. Ada ya malazi imeainishwa katika muundo wa ada ya chuo iliyoambatanishwa kwenye fomu hii.

Mahitaji ya Malazi kwa mwanafunzi

(i) Mto mmoja (ii) Mashuka mawili (iii) Chandarua kimoja (lazima).

Utapewa ufunguo mmoja wa chumba chako, kitanda na godoro. Vifaa vyote vilivyotolewa kwako pamoja na miundombinu ya mabweni vinapaswa kuangaliwa kwa uangalifu. Katika kesi ya hasara au uharibifu wowote utabeba gharama ya uharibifu. Vifaa vyote vilivyotolewa kwako lazima virudishwe kwa Msimamizi wa Majengo (Estate Manager) wakati wa kuondoka kwenye chumba chako. Kutofanya hivyo mwanafunzi atapaswa kulipa mali zote zilizopotea ama kutokabidhi na hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

**Huduma ya Chakula**

Misungwi CDTTI imetoa huduma za upishi kwa watu binafsi. Kwa hivyo, wanafunzi wanaweza kutumia migahawa hiyo kupata huduma ya chakula. Kwa hivyo, wanafunzi wanapaswa kupanga bajeti ya chakula kwa mwaka mzima wa masomo. Hii inalipwa kwa wanafunzi moja kwa moja kwa watoa huduma.

N.B. Ni marufuku kabisa kwa wanafunzi kupika katika vyumba vyao. Mwanafunzi yeyote atakayekiuka kanuni hii ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za wanafunzi.

### 7.2 Usafi wa Vyumba

Kazi ya kufagia na kuweka chumba chako kikiwa safi ni yako. Wasafishaji watasafisha vyoo na bafu pekee. Unatakiwa wakati wote kudumisha usafi wa jumla ndani na nje ya ya chumba na bweni.

## 8. Mahitaji ya Programu kwa wanafunzi (Departmental Students requirement) (wasiliana na Chuo kabla ya kufanya manunuzi)

- Scientific Calculator(Lazima)
- Safety boots – Black(lazima)
- Overcoat Dark Blue (lazima)
- Drawing Board A3 size(lazima muhula wa pili)
- Protractors
- Drawing Pens
- Drawing Compass (Mathematical Set)
- Triangle Templates
- Square Templates
- French Curves
- Laptop (Muhimu)
- Reflector (Lazima)
- Drawing Papers A3 size
- Fine liner

## 9. Serikali ya Wanachuo MISUNGWI CDTTI (MISO)

Wanafunzi wote wa MISUNGWI CDTTI ni wanachama wa Serikali ya wanafunzi wanapaswa kulipa Tzs 10,000/= kama ada ya uanachama kwa mwaka kupitia akaunti Na. **31310005698 NMB *MISUNGWI CDTTI Student's Organization (MISO)***

## 10. Maktaba, Kituo cha Kompyuta na Nyenzo za Kujifunzia

MISUNGWI CDTTI inatoa nyenzo mbalimbali za kujifunzia ikiwemo maktaba, maabara ya Kompyuta, Karakana za Ujenzi na Vifaa vingine vya kujifunzia. Pia kituo cha kompyuta kinashughulikia taarifa zote muhimu kuhusu programu za Uhandisi kama vile PRIMAVELA, AUTOCAD na ARCHCAD na kompyuta ZOTE zimeunganishwa na Mtandao (Wireless Internet).

## 11. Tamko Kuhusu Uzingatiaji wa Kanuni za MISUNGWI CDTTI

Wanafunzi wote waliokubali kujiunga na Misungwi CDTTI watatakiwa kusaini "Fomu ya Tamko la Wanafunzi" ambayo ni ahadi ya lazima kwa mwanafunzi anayehusika kuwa ataongozwa chini ya Sheria Ndogo za Misungwi CDTTI kuhusu Ustawi wa Jumla; Maadili; Nidhamu; Kesi za kinidhamu na Adhabu.

Hongera kwa kuchaguliwa na tunakukaribisha kwa moyo mkunjufu Misungwi CDTTI

MOTO: ***"Misungwi CDTTI – The Home of Engineers"***

Kwa maelezo zaidi:
**Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma – 0713197574/0743520523**
**Afisa Udahili1 – 0653118018**
**Afisa Udahili 2 - 0672566076**
**Baruapepe: pmissungwi@jamii.go.tz or misungwicdtti@gmail.com**
**Tovuti : www.misungwicdtti.ac.tz**

**Charles F. Achuodho**
**MKUU WA CHUO**

MISUNGWI COMMUNITY DEVELOPMENT TECHNICAL TRAINING INSTITUTE
PRINCIPAL
MWANZA

## Student Medical Examination Record Form

**The Medical form must be completed by the student and the Physical form completed by a Doctor. Forms must be returned to our office via hand delivered.**

**A. Medical History Form.**

**Demographic Information**

**Last name ………………… First name…………………………Middle name…………………….**

**Home address…………………………….Region……………………….District……………………………**

**Home phone:…………………… Alternate Phone…………………Email:………………………………..**

**Date of Birth……………………… Gender ……………………..**

**Please check (YES) and (NO) For each condition.**

| | YES | NO | | YES | NO | | YES | NO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Allergies | | | Joint problem | | | Malaria | | |
| Chills | | | Chest pain | | | Back pain | | |
| Paralysis | | | Cancer | | | Ear infections | | |
| Anemia | | | Depression | | | Heart Disease | | |
| Thyroid | | | Fainting | | | Vomiting | | |
| Asthma | | | Nervousness/panic | | | Chronic cough | | |
| fainting | | | Head injury | | | pneumonia | | |
| Bloodpressure | | | Sexually transmitted disease | | | Frequent Urinary track Infections | | |
| Ulcers | | | Sickle cell | | | | | |

**Are you allergic to any foods medications or other substances? Yes….No…. If yes, please list ……………………………………………………………………………………**

**Student signature ……………………………  Date .......................................**

**B. Physical Examination Form**

**Evaluations**

| Vital Signs | | | Laboratory Results and Immunizations Report | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Normal | Abnormal | Hct…………..<br>Hgb………….. | Normal | Abnormal |
| Blood pressure | | | | | |
| Temperature | | | Fasting blood pressure | | |
| Pulse | | | Urinalysis | | |
| Weight | | | Chest X ray<br>(only if TB is positive) | | |
| Height | | | | | |
| Mood | | | | | |

General appearance

| | normal | abnormal | | Normal | Abnormal |
|---|---|---|---|---|---|
| Eyes | | | Genitalia | | |
| Ears | | | Neurological | | |
| Nose | | | Muscular skeletal | | |
| Chest | | | | | |

List all known Allergies……………………………………………………………………………………………

Physical Activity Restriction Recommended? YES………NO…….
:………………………………………………

History of Surgery/Hospitalization
……………………………………………………………………………………

**Physician name and Signature** **Date** **Office stamp**
…………………………………… ……………. ………………………………………….

**(TUITION FEES AND OTHER CHARGES)**

| | | ITEM | SEMESTER I | SEMESTER II | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|
| | **TUITION FEE (ADA)** | | | | |
| | NTA LEVEL 4 (Basic technician certificate) | A | 300,000 | 300,000 | 600,000 |
| | NTA LEVEL 5 & 6 (Technician certificate and Ordinary Diploma) | A | 350,000 | 350,000 | 700,000 |
| | **OTHER CHARGES (MICHANGO MENGINE )** | | | | |
| | Registration fee (usajili) | B | 15,000 | - | 15,000 |
| | Identity card (kitambulisho ) | B | 10,000 | - | 10,000 |
| | Accommodation (malazi) | B | 100,000 | 100,000 | 200,000 |
| | Wear and tear (uchakavu )**non refundable** | B | 10,000 | - | 10,000 |
| | **Medical contribution NHIF (BIMA YA AFYA ) – NIDA Namba ni Muhimu awe nayo** | **B** | **50,400** | **-** | **50,400** |
| | First Aid (huduma ya kwanza) | B | 10,000 | - | 10,000 |
| | NACTE Quality Assurance fee | B | 15,000 | - | 15,000 |
| | Workshop practice fee | B | 65,000 | 65,000 | 130,000 |
| | Examination fee (mitihani) | B | 15,000 | 15,000 | 30,000 |
| | Certification (certificate &transcript) | B | - | 15,000 | 15,000 |
| | **TOTAL FOR NTA LEVEL 4** | A&B | **590,400** | **495,000** | **1,085,400** |
| | **TOTAL FOR NTA LEVEL 5 &6** | A&B | **640,400** | **545,000** | **1,185,400** |

# NAMNA YA MALIPO

## A: TUITION FEE (ADA):

Wanafunzi wote wanapaswa kulipa malipo ya ada kupitia Control Number zitakazoandaliwa na Mhasibu pindi mwanafunzi atakaporipoti chuoni kisha kupeleka Benki Tawi lolote au kwa malipo mitandao ya simu wasiliana na Mhasibu endapo kutakua na changamoto. **(+255767244694 au +255688409158)**

## B: **OTHER CHARGES (MALIPO MENGINE)**

Wanafunzi wote wanapaswa kulipa malipo mengine kupitia akaunti namba 31301100002 – CDTTI Mafunzo Account Misungwi NMB

***Zingatia: Mwanafunzi hatasajiliwa mapaka awasilishe risiti za malipo kama ushahidi wa malipo yake na Malipo ya mkononi hayatapokelewa***

## TAARIFA ZA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Majina kamili …………………………………………………………………………………

Tarehe ya Kuzaliwa ……………….Uraia ………..… Jinsia …………….

NIDA No……………………………………… **(lazima awe nayo wakati wa kuripoti chuoni)**
Sanduku la Posta: ………………………. Barua pepe: ………………………….
Namba za simu ………………………………../……………………
Wilaya ………………… Mkoa ………………….

**Taarifa za Mzazi/Mlezi/Mtu wa Karibu**
Jina kamili ………………………………………… Uhusiano …………….
Namba za simu ………………………………….……….… Sanduku la Posta………..
Baruapepe………………. …………
Wilaya ………………………… Mkoa …………………….

**Taarifa za Shule :**

Jina la Shule Msingi ……………………………………………….. mwaka uliomaliza …………

Wilaya …………………………… Mkoa ……………………….

Jina la shule ya Sekondari ……………………………..

Namba ya shule na mtihani ………………………..

Mwaka uliohitimu …………………………………..

---

### KUKUBALI KUJIUNGA NA KUTEKELEZA MASHARTI YOTE YA CHUO

Mimi ……………………………………………. Nimekubali masharti yote yaliyoainishwa hapo juu.

Nimepokea taarifa ya kuchaguliwa kujiunga na Misungwi CDTTI kwa fani ya Uhandisi Ujenzi na Maendeleo ya Jamii na nitahuduhuria mafunzo kwa kipindi chote nitakachokuwa chuoni ikiwemo kuhudhuria darasani, kushiriki mafunzo kwa vitendo na majaribio mbalimbali.

…………………….                                                    ……………

Sahihi ya Mwanafunzi                                                    Tarehe

**Zingatia: Fomu hii ijazwe kwa usahihi**